TANGAZO LA SERIKALI NA .................... la tarehe ...........................

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA 290)

# SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya kifungu 7(1) na 16(1)*

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MADINI YA UJENZI) (MAREKEBISHO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MISSENYI, 2017

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Ushuru wa Madini ya Ujenzi) za Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi (Marekebisho), 2017 na zitasomwa pamoja na Sheria Ndogo za (Ushuru wa Madini ya Ujenzi) za Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi 2011.

GN.No. 276 /2011

Tarehe ya kuanza kutumika

2. Sheria Ndogo hizi zitaanza kutumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi kuanzia tarehe ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Kufutwa kwa kifungu cha 4(2)

3. Kifungu cha 4(2) Sheria Ndogo kinafutwa na kuelezea kama ifuatavyo:-
4.- (2) Ada ya kuanzisha machimbo itakuwa ni Tsh.100,000/= ambazo zitalipwa kwa ajili ya usajili wa machimbo hayo kabla ya uchimbaji wa madini ya ujenzi.

Kufutwa kwa Jedwali

4. Jedwali la Sheria Ndogo linafutwa na badala yake litasomeka kama ifuatavyo:

*Jedwali la Kwanza*
*Limetengenezwa chini ya Kifungu cha 5*

**Ushuru wa Madini ya Ujenzi**

Kila tani itakayosombwa katika machimbo ya madini ya ujenzi italipiwa Tsh.1,000/=

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa katika Kikao cha Baraza la

Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi kilichofanyika tarehe …………………. na nembo hiyo ilibandikwa mbele ya-

………………………………..
***PROJESTUS K. TEGAMAISHO***
MWENYEKITI
HALMASHAURI YA WILAYA
YA MISENYI

………………………………
***LIMBE B. MAURICE***
MKURUGENZI WA
HALMASHAURI YA WILAYA
YA MISSENYI

NAKUBALI,

………………………………
***GEORGE B. SIMBACHAWENE (MB)***
WN OR - TAMISEMI

DODOMA

Tarehe ……………………………………..